# Kumwandikisha Mtoto Wako katika Jimbo la Ohio

## Uandikishaji

Kuanza kuhudhuria shule mpya ni wakati wa kusisimua kwa watoto na familia zao. Ni mwanzo wa mahusiano mapya na marafiki na walimu. Pia ni wakati ambapo familia yako inakuwa sehemu ya jumuiya ya shule. Kabla ya watoto wako kuanza kuhudhuria shule, ni lazima uwaandikishe. Wakati wa uandikishaji, utajifunza kuhusu mipango mingi na mambo ambayo shule inatoa kwa wanafunzi na familia.

Utahitaji kushiriki taarifa kuhusu familia yako na mtoto wako. Hii inajumuisha taarifa kuhusu uzoefu wa mtoto wako wa kuelewa na kutumia lugha nyingine ambazo si Kiingereza. Ikiwa mtoto wako alihudhuria shule katika nchi nyingine, ni muhimu kushiriki nyaraka zozote na zote ulizo nazo kutoka kwa shule zake za zamani, hata kama zimeandikwa katika lugha nyingine.

> Shule zinaweza kuomba familia zilete nyaraka za shule zilizotafsiriwa wakati wa kuandikisha mtoto wao katika shule mpya. Katika hali hizi, huenda familia zikahitaji kulipa ada ili kupata nakala zilizotafsiriwa. Baadhi ya mashirika ya jamii yanaweza kutoa huduma za tafsiri kwa gharama ya chini au bure.

Familia yako ina haki muhimu wakati wa kumwandikisha mtoto wako shuleni. Kwa mfano, shule haziwezi kulazimisha au kuhitaji familia zitoe nambari zao za usalama wa kijamii. Pia haziwezi kuhitaji familia ziseme hali zao za uhamiaji kama mahitaji ya watoto kuandikishwa au kuhudhuria shule. Ili ujifunze zaidi kuhusu haki za familia na wanafunzi, tembelea sehemu yetu ya haki za elimu.

> **Unaweza pia kutazama video kuhusu Kumwandikisha Mtoto Wako katika Jimbo la Ohio.**

## Je, mtoto wangu anapaswa kuandikishwa shuleni wakati gani?

Nchini Marekani, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Hii inawapa watoto maarifa na ujuzi wanaohitaji ili wafanikiwe katika siku zijazo. Kwa sababu hiyo, kuna sheria nchini Marekani

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

zinazohitaji familia ziwaandikishe watoto wao shuleni. Watoto wote wanaoishi katika jimbo la Ohio wanatakiwa kupata elimu kuanzia umri wa miaka 6 hadi 18.

> Wanafunzi ambao ni wanafunzi wa Kiingereza wanaweza kuhudhuria shule ya upili hadi wanapofikisha umri wa miaka 22.

Katika Ohio, kuna machaguo ya watoto wadogo ya kuhudhuria mipango ya mafundisho ya mapema au shule ya awali kabla ya kusajiliwa katika shule ya chekechea. Lazima mtoto awe na umri wa miaka 5 ili aweze kujiunga na shule ya chekechea au umri wa miaka 6 li aweze kujiunga na darasa la kwanza. Umri wa mwisho ambao mtoto anaweza kuandikishwa katika shule ya chekechea ni hadi umri wa miaka 6. Watoto wengi huanza elimu yao katika shule ya chekechea wakiwa na umri wa miaka 5 au 6 na huwa wanahitimu baada ya darasa la 12 wakiwa na umri wa miaka 17 au 18. Kila ngazi ambayo wanafunzi hupitia shuleni inaitwa darasa.

- Ikiwa familia yako ni wageni nchini Marekani au katika jimbo la Ohio na mliwasili huko katika majira ya joto, jaribu kumwandikisha mtoto wako kabla ya mwanzo wa mwaka mpya wa masomo. Kwa kawaida, mwaka wa masomo huanza katika mwezi wa Agosti au Septemba.
- Familia yako ikiwasili kutoka katika jimbo au nchi nyingine baada ya mwaka wa masomo kuanza, mwandikishe mtoto wako haraka iwezekanavyo.
- Ikiwa mtoto wako anabadilisha kutoka shule moja ya Ohio hadi nyingine, mwandikishe mtoto wako katika shule hiyo mpya haraka iwezekanavyo.

> Kwa kawaida, mwaka wa masomo huanza katika mwezi wa Agosti hadi Mei. Kwa kawaida, wanafunzi huwa kwenye mapumziko mnamo Desemba na Januari na katika miezi ya majira ya joto. Watoto huwa hawahudhurii shule wakati wa likizo maalum na mapumziko. Tarehe hizi huchaguliwa na kila wilaya ya shule. Kwa kawaida, watoto huwa wanahudhuria shule siku tano kwa wiki kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Jifunze zaidi kuhusu mfumo wa shule wa Marekani kwenye ukurasa wa Shule ya Umma ya USA Hello.

Baada ya mtoto wako kuandikishwa shuleni, anatarajiwa kwenda shuleni na kushiriki katika madarasa kila siku ya masomo. Watoto wanaohudhuria shule kila siku wana uwezekano mkubwa wa kufaulu shuleni na kuhitimu kwa wakati unaofaa. Tembelea sehemu yetu ya mahudhurio ili ujifunze zaidi.

Wazazi huko Ohio wanaweza kuchagua kuwasomesha watoto wao nyumbani badala ya kuwapeleka shuleni. Wanahitaji tu kumwambia msimamizi mkuu wa wilaya ya shule wa eneo lao na kufuata sheria za Ohio za mafundisho ya nyumbani. Jifunze zaidi kwenye ukurasa wa Mafundisho ya Nyumbani kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce).

## Kuwaandikisha Watoto Walio na Umri wa Chini ya Miaka Sita

### Shule ya awali

Watoto wenye umri wa miaka 3 hadi 5 wanaweza kuhudhudia shule ya awali. Shule ya awali pia inaweza kuwasaidia watoto wanaohitaji usaidizi wa ziada wa kujifunza kupata msaada wanaohitaji. Hii inamaanisha kwamba shule ya awali haihitajiki. Shule ya awali inaweza kuwasaidia watoto kukuza ujuzi muhimu na kijitayarisha kwa shule ya chekechea. Familia zinaweza kuchagua wakati na mahali ambapo watoto wao watahudhuria shule ya awali. Jifunze mambo mengi zaidi kuhusu shule ya awali kwenye tovuti ya Colorín Colorado.

#### Shule ya awali inaweza kuwasaidia watoto:

- Kujitayarisha kwa shule ya chekechea.
- Kukuza ujuzi muhimu wa kijamii na kihisia.
- kushiriki katika shughuli zinazosaidia ukuaji wao.
- Kuwa na nia na kutaka kujifunza.
- Kujifunza jinsi ya kujitunza wenyewe na kuwatunza watu wengine.
- Kujifunza stadi za kuwatayarisha kusoma na kufanya hesabu.
- Kuboresha uwezo wao wa kufikiri na stadi za lugha.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

## Shule ya Chekechea, ngazi ya kwanza shuleni

Watoto wanaweza kuanza kupata elimu rasmi mapema kuanzia umri wa miaka 5. Huwa wanaanza kwa kuhudhuria ngazi ya kwanza ya kupata elimu rasmi nchini Marekani, ambayo ni shule ya chekechea. Umri wa mwisho ambao mtoto anaweza kuandikishwa katika shule ya chekechea ni akiwa na umri wa miaka 6. Ili watoto waweze kuhudhuria shule ya chekechea, lazima wawe na umri wa miaka 5 ifikapo tarehe mahususi. Tarehe hii inaweza kuwa tofauti katika kila wilaya ya shule.

> Ni muhimu kuuliza wilaya yako ya shule ili ujue wakati ambapo unaweza kumwandikisha mtoto wako na mambo unayohitaji kufanya. Katika baadhi ya wilaya za shule, watoto lazima wafikishe umri wa miaka 5 ifikapo tarehe 1 Agosti au tarehe 30 Septemba ili waweze kuandikishwa shuleni. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu shule ya chekechea kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce).

- Katika shule ya chekechea, watoto hujifunza kusoma na kuandika maneno na sentensi za msingi.
- Pia huwa wanakuza ujuzi wao wa hisabati kwa kujifunza kuhesabu, kujumlisha, na kutoa tarakimu ndogo.
- Watoto hushiriki katika shughuli mbalimbali za mikono, kama vile uchoraji, kuchora, na kujenga kwa kutumia vitalu ili kukuza ubunifu wao.
- Huwa wanajifunza kutangamana na kujihusisha na marika zao kupitia kucheza michezo na kushiriki katika vikundi.
- Wanafunzi wa shule ya chekechea pia huanza kukuza ujuzi wao wa mwendo wa misuli midogo kupitia shughuli kama vile kukata, kupaka rangi, na kutumia mikasi.

Jifunze zaidi kuhusu shule ya awali na shule ya chekechea kwenye ukurasa wa Rasilimali za Familia za Mafundishio ya Mapema za tovuti ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce).

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Hatua za Kumwandikisha Mtoto Wako Shuleni

Ili umwandikishe mtoto wako shuleni katika darasa lolote unahitaji kufuata baadhi ya hatua.

1. **Kubainisha wilaya ya shule inayohudumia familia mahali ambapo unaishi.** Unaweza kutembelea ukurasa wa Kutafuta wa tovuti ya Idara ya Ushuru ya Ohio (Ohio Department of Taxation) ili ujue wilaya yako ya shule. Ingiza tu anwani yako ya nyumbani. Familia katika Ohio zinaweza kuchagua mahali ambapo watoto wao watahudhuria shule. Machaguo huwa tofauti kulingana na mahali ambapo familia zinaishi. Ili kujifunza kuhusu aina tofauti za shule katika Ohio, tumia Zana ya Ohio ya Kuchagua Shule kwenye tovuti ya Kituo cha Ushiriki wa Familia cha Jimbo Nzima la Ohio (Ohio Statewide Family Engagement Center).
2. **Kuwasiliana na wilaya ya shule ili kujua jinsi unavyoweza kumwandikisha mtoto wako.** Shule zinaweza kuambia familia ziwaandikishe watoto wao mtandaoni au ana kwa ana. Baadhi ya wilaya za shule zinaweza kukuambia uende katika shule ya eneo lako au katika kituo kuu cha uandikishaji katika wilaya ya shule. Unaweza kupata nambari za simu na anwani za wilaya kwenye tovuti ya wilaya. Unaweza pia kutembelea ofisi za wilaya ili uulize ana kwa ana. Kwa wakati huu, unaweza kujulisha wilaya ya shule ikiwa unahitaji mkalimani. Mkalimani anaweza kukusaidia kuzungumza na shule wakati unamwandiksiha mtoto wako.
3. **Kukamilisha shughuli za uandikishaji za wilaya ya shule.** Wakati mwingine, unaweza kufanya shughuli hizi ana kwa ana au mtandaoni.
4. **Ili umwandiksihe mtoto wako, utahitaji kupatia wilaya ya shule taarifa kuhusu mtoto na familia yako.** Baadhi ya nyaraka na taarifa ambayo utahitaji kupatia wilaya ni nyaraka zinazoonyesha:
    - Umri wa mtoto wako.
    - Anwani ya familia yako katika wilaya hiyo ya shule.
    - Rekodi ya mtoto wako ya kupokea chanjo zinazohitajika.
    - Taarifa kuhusu wazazi au walezi wa mtoto wako.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

- Lugha unayopenda.

5. **Kuthibitisha kuwa una taarifa unayohitaji kutoka shuleni ili mtoto wako aweze kuanza kuhudhuria shule.**
6. **Kuhakikisha kuwa unauliza maswali yoyote uliyo nayo.**
7. **Kushiriki taarifa yoyote ambayo ungependa shule ijue kuhusu mtoto wako au familia yako.**

## Orodha ya Ukaguzi ya Nyaraka Unazohitaji kwa ajili ya Uandikishaji

Orodha hii ya ukaguzi inajumuisha nyenzo ambazo shule nyingi huhitaji ili kuwaandikisha wanafunzi. Nyenzo zinazohitajika au kukubaliwa zinaweza kuwa tofauti katika kila shule. Ni muhimu kuuliza shule kuhusu aina za nyaraka na nyenzo zinazonahitajika kutoka kwa familia yako.

### ☐ Nyenzo za Utambulisho kutoka kwa Wazazi au Walezi

Baadhi ya machaguo ni pamoja na:

- Leseni ya dereva.
- Picha ya utambulisho kutoka nchini Marekani.
- Kadi ya kijani.
- Pasipoti.
- Viza.
- Fomu ya I-94.

### ☐ Nyaraka Zinazoonyesha Tarehe Ambayo Mtoto Wako Alizaliwa

Baadhi ya machaguo ni pamoja na:

- Cheti cha kuzaliwa.
- Pasipoti inayoonyesha tarehe na mahali pa kuzaliwa.
- Kumbukumbu ya kidini iliyothibitishwa inayoonyesha tarehe na mahali pa kuzaliwa.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

- Hati ya kiapo ya kuzaliwa.

## ☐ Nyaraka Zinazoonyesha Kuwa Familia Yako Inaishi Katika Wilaya Hiyo ya Shule

Baadhi ya machaguo ni pamoja na:

- Bili ya huduma ya hivi karibuni (gesi, umeme, maji) iliyotumwa kwa anwani yenye jina la mzazi au mlezi.
- Karatasi ya hivi karibuni ya mshahara na makato yake yenye jina na anwani ya mzazi au mlezi.
- Mkataba wa sasa wa kupangisha nyumba wenye jina la mzazi au mlezi.

## ☐ Nyaraka Zinazoonyesha Kuwa Mtoto Wako Amepata Chanjo Zinazohitajika

Huenda shule ikahitaji chanjo hizi au chanjo na vipimo vingine:

- Dondakoo, Pepopunda, na Kifaduro (DPT).
- Ugonjwa wa Polio (IPV).
- Surua, Matumbwitumbwi, na Rubella.
- Mchochota wa ini aina ya B.
- Tetekuwanga.
- Meningokokasi (kwa wanafunzi wa madarasa ya 7 na 12).
- Kipimo hasi cha kifua kikuu (kwa wanafunzi waliozaliwa nje ya Marekani au waliosafiri kwenda nchi nyingine hivi karibuni).

Unaweza kujifunza zaidi kuhusu chanjo zinazohitajika kwa watoto wenye umri tofauti kwenye tovuti ya Idara ya Afya ya Ohio (Ohio Department of Health).

Ikiwa hutaki kumchanja mtoto wako kwa sababu za kidini au sababu nyingine, zungumza na shule, au uliza kuhusu suala hili unapomwandikisha mtoto wako.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

### ☐ Taarifa kutoka katika Shule ya Zamani, ikiwa Inapatikana

Machaguo ni pamoja na:

- Nyaraka za elimu maalum, kama vile Mpango wa Elimu wa Mtu Binafsi (Individual Education Plan (IEP), mpango wa 504, au Ripoti ya Timu ya Tathmini.
- Kumbukumbu ya mahudhurio.
- Nakala ya matokeo ya mitihani (alama alizopata katika shule ya zamani).
- Alama za mtihani au tathmini.

## Fomu na Taarifa za Uandikishaji

Baadhi ya wilaya za shule zina fomu za uandikishaji ambazo huwa zinaomba familia zijaze wakati wa kuwaandikisha watoto wao. Fomu na njia ambazo shule hutumia kukusanya taarifa ya mwanafunzi huenda zikawa tofauti. Shule ambapo unamwandikisha mtoto wako inapaswa kukueleza kuhusu fomu unazohitaji kujaza.

- ☐ **Fomu ya mtu wa kuwasiliana naye wakati wa dharura** - Shule inaweza kukuomba utoe taarifa kuhusu mtu mmoja au watu wengi ambao inaweza kuwasiliana nao wakati wa dharura ikiwa haiwezi kuwasiliana na wazazi au walezi.
- ☐ **Utafiti wa Lugha ya Nyumbani** - Fomu hii hutumiwa na shule ili kuelewa lugha inayozungumzwa nyumbani na lugha ambayo familia yako inaelewa vizuri. Taarifa hii pia husaidia shule kujua ikiwa mtoto wako anaweza kufaidika akipata msaada wa kuboresha ujuzi wake wa Kiingereza.
- ☐ **Kumbukumbu za wanafunzi kutoka kwa shule ya zamani** - Wanafunzi wanaojiandikisha katika wilaya mpya ya shule wanaweza kuombwa watoe taarifa kutoka kwa shule zao za zamani. Hii inaweza kujumuisha taarifa kuhusu alama zao, mahudhurio, na alama za mtihani.
- ☐ **Nyaraka za elimu maalum** - Familia zilizo na watoto waliopata huduma ya elimu maalum katika shule zao za zamani zinaweza kuombwa zitoe taarifa kuhusu Mpango wa Elimu wa

Mtu Binafsi (Individualized Education Plan (IEP)) wa watoto, Ripoti ya Timu ya Tathmini, au mpango wa 504.

- **Utafiti wa taarifa ya wanafamilia** - Utafiti huu unaweza kuomba taarifa kuhusu familia yako na mapato ya wanafamilia wako. Shule inaweza kukuuliza kuhusu kiasi cha fedha ambacho familia yako hupata. Swali hili huulizwa ili kujua ikiwa familia yako au mtoto wako anaweza kupata msaada wa ziada.
- **Fomu ya chakula cha bure na cha bei iliyopunguzwa** - Wakati wa uandikishaji, shule inaweza kuomba familia itoe taarifa hii. Taarifa hii hutumiwa kujua ikiwa mtoto wako anaweza kupata chakula cha bure au cha bei iliyopunguzwa kutoka shuleni. Shule inaweza pia kuuliza kuhusu kiasi cha fedha ambacho familia yako hupata.
- **Fomu za usafiri** - Wakati wa uandikishaji, shule inaweza kuomba familia itoe taarifa ili ijue ikiwa mtoto wako anahitaji msaada wa kwenda shuleni. Shule inaweza kuuliza kuhusu watu wanaoruhusiwa kumchukua mtoto wako kutoka shuleni.
- **Fomu za Ulinzi** - Mtoto anaweza kuishi na mtu mwingine ambaye si mzazi wa kibiolojia au na wazazi ambao wametengana au waliopata talaka. Shule inaweza kuomba nyaraka zinazothibitisha kuwa mtu ana mamlaka ya kisheria ya kumlinda mtoto.

## Vidokezo na Maswali ambayo Familia Zinaweza Kuuliza Wakati wa Uandikishaji

Shule inaweza kukuomba taarifa nyingi. Huu pia ni wakati mzuri wa kujifunza kuhusu shule. Unaweza kuuliza maswali ambayo yatakusaidia wewe na mtoto wako. Hapa kuna orodha ya maswali unayoweza kuuliza.

### Maswali Unayoweza Kuuliza Wakati wa Uandikishaji

- Je, shule inaweza kumsaidia mtoto wangu kujifunza Kiingereza vipi?
- Nitapataje taarifa kutoka shuleni baada ya mtoto wangu kuandikishwa?
- Je, shule inaweza kunisaidia kumfikisha mtoto wangu shuleni au nyumbani?
- Je, shule ina mipango ya kabla au ya baada ya shule? Je, nitamwandikisha mtoto wangu

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

katika mipango hii vipi?

- Mtoto wangu hutumia dawa wakati wa mchana. Ninawezaje kuhakikisha kuwa mtoto wangu huwa anatumia dawa hizo akiwa shuleni?
- Ninaweza kupata wapi taarifa kuhusu chakula kinachotolewa na shule?
- Je, shule inahitaji sare au ina kanuni ya mavazi?
- Je, saa za shule ni saa ngapi?
- Je, kuna kalenda ya shule inayoonyesha likizo na wakati wa mapumziko ya shule?
- Ninaweza kufanya nini ikiwa familia yangu husherehekea likizo ambayo haijajumuishwa kwenye kalenda ya shule?
- Je, mtoto wangu anahitaji vifaa gani vya shule kwa siku chache za kwanza za shule?

## Vidokezo kwa Familia

- Unapopanga miadi ya kumwandikisha mtoto wako, ijulishe shule ikiwa ungependa huduma ya usaidizi wa mkalimani.
- Hakikisha kuwa umeambia shule kuhusu mizio, hali za matibabu, au dawa zozote ambazo mtoto wako anahitaji.
- Ikiwa inawezekana, tembelea tovuti za shule na wilaya yako ili uone taarifa inayopatikana inayoweza kukusaidia kujitayarisha kumwandikisha mtoto wako.
- Omba kalenda ya shule na taarifa kuhusu wakati ambapo shule inaweza kuchelewa kufunguliwa au kufungwa mapema.

## Rasilimali za Ziada

- Ukurasa huu wa USA Hello hutoa taarifa zaidi kuhusu jinsi shule zinavyofanya kazi nchini Marekani https://usahello.org/education/children/public-school
- Ukurasa huu wa usajili wa shule kutoka USA Hello hutoa taarifa ya ziada ya uandikishaji katika lugha tofauti. https://usahello.org/education/children/register-child-in-schoo
- Zana hii ya Familia ya Mwanafunzi wa Kiingereza inapatikana katika lugha nne (Kiingereza, Kiarabu, Kichina na Kihispania) na inajumuisha taarifa kuhusu uandikishaji. Fuata tu kiungo hiki na uchague Sura
- https://ncela.ed.gov/educator-support/toolkits/family-toolkit

(https://ncela.ed.gov/educator-support/toolkits/family-toolkit)

- Hati hii yenye taarifa kuhusu jinsi ya kumwandikisha mtoto shuleni kutoka katika Kituo cha Sheria ya Elimu inaelezea jinsi ya kuwaandikisha watoto wanaoishi na mtu mwingine ambaye si wazazi wao. https://www.elc-pa.org/wp-content/uploads/2021/08/how-to-enroll-a- child-living-with-caregivers-1302-fact-sheet.pdf (https://www.elc-pa.org/wp-content/uploads/2021/08/how-to-enroll-a-child- living-with-caregivers-1302-fact-sheet.pdf)
- Ukurasa huu wa tovuti wa Idara ya Afya ya Ohio (Ohio Department of Health) unaelezea kuhusu chanjo ambazo wanafunzi wanahitaji ili waweze kuhudhuria shule. https://odh.ohio.gov/know-our-programs/immunization/media/immunization-summary- Shule (https://odh.ohio.gov/know-our-programs/immunization/media/immunization-summary-school)
- Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) inayoendesha ukurasa wa wavuti wa wanafunzi wanaozungumza lugha mbili inaelezea kuhusu mchakato wa utambulisho. https://education.ohio.gov/Topics/Early-Learning/Supporting-Young-Dual-Language-Learners

*Rasilimali hizi zinalenga kuimarisha masomo, ustawi wa wanafunzi, na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa Ohio wanaozungumza lugha nyingi. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi za kushirikiana kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) na Kituo cha Chuo Kikuu cha Jimbo la Ohio cha Elimu na Mafunzo ya Kazi (The Ohio State University's Center on Education and Training for Employment) pamoja na kikundi cha kujitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 